



**KIRIRI WOMEN'S UNIVERSITY OF SCIENCE AND TECHNOLOGY  
KISW 2201 - LANGUAGE SKILLS IN KISWAHILI**

**UNDERGRADUATE UNIVERSITY EXAMINATIONS**

**SCHOOL OF EDUCATION**

**DEGREE OF BACHELOR OF ARTS IN EDUCATION**

**KISW 2301 - CURRENT ISSUES IN THE STUDY OF KISWAHILI**

**DATE: DEC 2023**

**DURATION: .**

**MAXIMUM MARKS: 70**

**MAAGIZO:**

1. Andika nambari yako ya usajili katika kitabu cha majibu ulichopewa.
2. **USIANDIKE CHOCHOTE** kwenye karatasi ya maswali
3. Karatasi hii ya mtihani ina maswali **TANO(5)**
4. **SWALI LA KWANZA** ni la lazima
5. Jibu maswali mengine **MAWILI** kutoka sehemu zilizobaki.
6. **SWALI LA KWANZA** lina alama **30** ilhali maswali mengine yana **ALAMA 20** kila moja.
7. **Jibu majibu yako yote katika kitabu cha majibu/ mtihani ulichopewa.**
- 8.

**SWALI LA KWANZA****(alama 30)**

1. a) Tofautisha kati ya dhana zifuatazo kuhusu lugha kwa kutolea mifano mwafaka:

i) lugha ya taifa **(alama 03)**

ii) lugha ya kitaifa **(alama 03)**

iii) lugha ya kimataifa **(alama 03)**

b) Kwa kurejelea hoja **sita**, dhibitisha kuwa Kiswahili ni Lugha ya kitaifa. **(alama 06)**

c) Utayarishaji na uchapishaji wa magazeti kwa lugha ya Kiswahili nchini Kenya umegubikwa na changamoto anuwai. Zibainishe changamoto hizi na upendekeze usuluhishaji wa changamoto hizo. **(alama 10)**

d) Jadili hoja tano kuonyesha ni vipi Kiswahili kinaweza kutumiwa kuwasilisha na kuangazia suala la mabadiliko ya tabia nchi kama suala ibuka duniani. **(alama 05)**

**SWALI LA PILI****(alama 20)**

2. a) Kwa kutolea hoja **tano**, jadili nafasi ya Kiswahili kama chombo cha mawasiliano ya umma nchini Kenya. **(alama 10)**

b) Pambanua taasisi tano zinazochangia katika kukikua na kukiendeleza Kiswahili nchini Kenya. **(alama 05)**

c) Jadili masuala ibuka **matano** yanayoweza kuanganizwa katika lugha ya Kiswahili katika ulimwengu wa sasa. **(alama 05)**

**SWALI LA TATU****(alama 20)**

3. a) Tofautisha kati ya dhana ya **sera ya lugha** na **usanifishaji wa lugha**. **(alama 04)**

b) 'Sera ya lugha nchini Kenya hutekeleza jukumu la kipekee katika kuikuza lugha.' Jadili rai hii kwa kurejelea hoja **tatu**. **(alama 06)**

c) Onyesha ni kwa namna gani Kiswahili kinatumiwa katika wavuti na mitandao ya kijamii kulegeza mipaka ya kitabaka na kikabila. **(alama 10)**

**SWALI LA NNE****(alama 20)**

4. a) Upangaji lugha ni nini **(alama 02)**

b) Kwa kurejelea hoja **nne**, onyesha umuhimu wa upangaji lugha. **(alama 04)**

- c) Pambanua mawanda mawili makuu yanayotumiwa katika upangaji lugha. **(alama 04)**
- d) “Licha ya kuwa matumizi ya Kiswahili yamepiga hatua kubwa katika mitandao ya kijamii, lugha ya Kiswahili bado imekumbwa na changamoto si haba katika mawanda hayo ya kiteknolojia.” Jadili rai hii. **(alama 10)**

**SWALI LA TANO(alama 20)**

5. a) Fafanua sababu saba zilizofanikisha maenezi ya Kiswahili nchini Kenya baada ya uhuru. **(alama 07)**
- b) Jadili mielekeo hasi saba inayoathiri lugha ya Kiswahili miongoni mwa wakenya nchini Kenya. **(alama 07)**
- c) Katika jumuiya ya Afrika ya Mashariki, Kiswahili kinatumika kama Lingua Franka. Jadili sifa **sita** zinazokifanya Kiswahili kuwa na hadhi ya lingua Franka. **(alama 06)**